

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA LIWALE

SHULE YA SEKONDARI HANGAI,
S.L.P 197,
LIWALE.
LINDI.

JINA LA MWANAFUNZI
SHULE YA MSINGI

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA
SEKONDARI HANGAI 2021
(JOINING INSTRUCTIONS)

Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari- Hangai Liwale. Fahamu ya kuwa umepata bahati ya pekee ya kuendelea na masomo ya sekondari wakati wenzako wengi wameikosa, hivyo yakubidi uitumie vema nafasi hii kwa manufaa yako, Familia yako, jamii yako na Taifa kwa ujumla. Weka juhudi kubwa katika tabia njema na masomo yako.

Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **11/01/2021** bila kukosa.

Shule ipo Kijiji cha **NGUNJA** kata ya **Ngongowe** umbali upatao kilomita 48 kutoka Liwale mjini, barabara ya kwenda Lilombe. Shule hii ni ya kutwa hivyo kama mzazi unatakiwa kumpangishia mwanao chumba hapa NGUNJA na kumpa mahitaji yote ya muhimu ili aweze kuhudhuria shuleni kikamilifu, Hii ni kwa wazazi wa watoto wanaotokea vijiji vya jirani yaani **LILOMBE, LILOMBE B,NGONGOWELE NA MIKUYU**. Pamoja na maelezo haya katika fomu hii naambatanisha viambatanisho vifuatavyo;

- (i) Nakala yenye mahitaji ya shule kiambatisho A.
- (ii) Nakala yenye hati ya tabibu au daktari kuhusu afya yako (medical examination form) (kiambatisho B).
- (iii) Nakala yenye sheria za shule (kiambatisho C)
- (iv) Nakala yenye maelezo binafsi ya kutoshiriki katika mgomo,fujo na makosa ya jinai (kiambatisho D)
- (v) Nakala yenye maelezo ya mzazi/mlezi ya kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelezo mengine ya shule (kiambatisho E)

NB:Unapofika shule uje na fomu hii pamoja viambatisho B,D na E vikiwa vimejazwa kwa ukamilifu.

Kwa mawasiliano na mkuu wa shule piga: [0620598656](tel:0620598656)

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI HANGAI

.....
PROSPER K. TAMASHA
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI HANGAI

MAHITAJI YA SHULE

A. SARE YA SHULE

(i) WAVULANA.

1. Suruari ndefu 2 za kushona rangi ya kaki (urefu wa heshima na isabane)
2. Mashati meupe 2 mikono mifupi.(Tomato)
3. Viatu vyeusi vyenye kamba na soksi nyeupe jozi 2
4. Mkanda mweusi wa ngozi (Usiwe wa utambi)
5. Vesti cheupe kwa ajili ya kuvaa ndani ya shati ya shule
6. Suruali rangi ya bluu bahari kwa ajili ya kushindia

(ii) WASICHANA

1. Sketi 2 ndefu zinazovuka magoti rangi ya kijani na zifunike ugoko wote(mshono linda box)
2. Viatu vyeusi vyenye kamba na soksi nyeupe jozi 2 (Asije na bajaji)
3. Mashati 2 meupe mikono mifupi (tomato)
4. Kitop cheupe kwa ajili ya kuvaa ndani ya shati ya shule
5. Juba jeupe kwa waislamu

B. VIFAA VYA MASOMO

1. Mdaftari makubwa 11 (counter book)
2. Kalamu za kutosha
3. Rula ya sentimita 30
4. Kibwete (Mkebe)
5. Kamusi ya Kiswahili na Kiingereza(lazima kila mmoja awe nayo)
6. Mkoba wa kuchukulia vifaa vya darasani(begi)
7. Saa ya mkononi inayofanya kazi
8. Leso

C. NGUO ZA MICHEZO

WAVULANA

1. Bukta na fulana rangi ya bluu
2. Viatu na soksi ndefu za michezo

WASICHANA

1. Traki na fulana rangi ya blue
2. Raba za michezo na soksi

D. VIFAA VYA USAFI

1. Aje na mfagio (chelewa)
2. Aje na jembe lenye mpini(ngwamba) na panga, vyote viwe vipya

E. VIFAA VINGINE

1. Aje na karatasi nyeupe(Rim paper aina ya A4) kwa ajili ya mitihani mbalimbali.

LIWALE DISTRICT COUNCIL

From,
The headmaster,
Hangai secondary school
P.O. Box 197,
Liwale

Date

To:
The medical officer,
Liwale District Hospital/Ngunja/Lilombe/Ngongowele Dispensary
P.O.BOX
LIWALE .

REF:.....(NAME IN FULL).

Please examine the named person and certify his/her physical and mental fitness for being a student. Attention should be paid to the following categories:

- a. Eye (sight).....
- b. Hearing.....
- c. Limbs.....
- d. Speech.....
- e. Leprosy.....
- f. Epilepsy.....
- g. Neurosis.....
- h. Pregnancy.....
- i. Sexual transmitted diseases
- j. Other serious diseases

Yours faithfully,

.....
PROSPER K. TAMASHA
HEADMASTER
HANGAI SECONDARY SCHOOL

MEDICAL CERTIFICATE (To be completed by a Government medical officer of authorized medical personnel)

I have examined the named person and here by certify that findings above are correct and that the person is fit/unfit to undergo secondary school studies.

.....
SIGNATURE & OFFICIAL STAMP

.....
DATE

SHERIA ZA SHULE

Kila mwanafunzi ni lazima;

- 1) Aheshimu wakubwa na wenzake
- 2) Akimbie mara baada ya kuitwa na mzazi au mlezi shuleni.
- 3) Atii kengere na kufuata ratiba vizuri
- 4) Avae sare na mavazi mengine kwa heshima
- 5) Aombe ruhusa kabla ya kuondoka shuleni kama ana dharura au sababu nje ya maeneo ya shule
- 6) Aonane na kuongea na wageni baada ya kupata ruhusa ya mwalimu wa zamu au mlezi husika.
- 7) Awepo darasani wakati wote wa vipindi na ashiriki kazi zote za usafi au za mikono.
- 8) Awe mtii kwa uongozi wa serikali ya shule na serikali ya wanafunzi (viranja wa shule).
- 9) Aongee lugha ya kiingereza wakati wote wa masomo (akiwa ndani ya eneo la shule).
- 10) Awe mlinzi na mtunzaji wa mali za umma.
- 11) Asimame na kuamkia wakati wazazi/walezi/walimu na wafanyakazi wanaopita karibu naye.
- 12) Asikose vipindi zaidi ya 45 mfululizo
- 13) Kukiuka sheria, kanuni au utaratibu zilizotajwa hapo juu zitampelekea mkiukaji kuadhibiwa adhabu za kawaida bila kufukuzwa shule.

NB: Mwanafunzi akiharibu au kupoteza mali yoyote ya shule kama viti,meza,vifaa vya maabara na miundo mbinu mingine mwanafunzi huyo na mzazi wake watawajibika kulipa.

MAKOSA YA KUFUKUZWA SHULE BILA MJADALA;

1. Wizi
2. Uasherati,Ubakaji, Ushoga na Kufumaniwa ugoni
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, Kubeli nk.
4. Uvutaji bangi na makosa ya jinai (kuuwa, kubaka n.k)
5. Kupigana na kupiga
6. Kuoja na kuolewa
7. Kudharau bendera ya taifa au kutembea wakati wimbo wa Taifa unaimbwa.
8. Kuwa mtoro zaidi ya siku 90 bila sababu au taarifa yeyote.
9. Kugoma au kukataa adhabu makusudi
10. Kupata, kutia na kutoa mimba.
11. Kushiriki kwenye kumbi/maeneo ya starehe kama vilabu vya pombe, mziki, bar, disko, ngoma za asili n.k
12. Kugomea, kushiriki na kuchochea mgomo na vurugu

Hatua zitachukuliwa ukifanya ndani ya eneo la shule au nje ya eneo la shule.

KIAMBATISHO-D

MWANAFUNZI

MKATABA WA KUTOSHIRIKI MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.

Mimi

Wa kidato cha kwanza 2020 katika shule ya sekondari Hangai nimesoma na kuelewa sheria na taratibu za shule yangu, hivyo ninaahidi kuwa nitafuata sheria, kanuni na taratibu zote zilizopo katika **KIAMBATISHO C** (Sheria za shule) na ninatambua kuwa iwapo nitakiuka taratibu yeyote ile itanipelekea kupata adhabu, kusimamiswa masomo au kufukuzwa shule.

Nakiri kuwa iwapo nitakiuka taratibu na sheria zilizoelezwa kwenye fomu ya sheria nichukuliwe hatua stahiki.

SAINI YA MWANAFUNZI

JINA LA MWANAFUNZI

TAREHE

KIAMBATISHO -E

MZAZI

**MAELEZO YA KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO
YATAKAYOTOLEWA NA SHULE.**

Mimimzazi/mlezi

wa

wa kijiji cha.....

Ninakili na ninakubaliana na sheria, kanuni zilizoelezwa katika **KIAMBATISHO C** inayoonyesha sheria, kanuni na taratibu zote za shule na pia nitafuata maelekezo mengine yatakayotolewa na shule pamoja na kuyatekeleza kama yatakavyoagizwa na uongozi wa shule.

Hivyo iwapo mtoto wanguakikiuka taratibu na kanuni za shule achukuliwe hatua za kinidhamu kama zilivyoenezwa kwenye fomu ya sheria za shule.

Jina la Mzazi/Mlezi.....

Mzazi/Mlezi wa.....

Saini ya Mzazi/Mlezi

Tarehe